JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2024

## KISWAHILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2024

# 021 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2025**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI ......................................................................................iv

1.0 UTANGULIZI ......................................................................................1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ......................................................................................2

2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA ......................................................................................2

2.1.1 Swali la 1: Kuchagua ......................................................................................2

2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha ......................................................................................13

2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ......................................................................................16

2.2.1 Swali la 3: Ufahamu ......................................................................................17

2.2.2 Swali la 4: Uundaji wa Maneno ......................................................................................23

2.2.3 Swali la 5: Uundaji wa Maneno ......................................................................................28

2.2.4 Swali la 6: Mawasiliano ......................................................................................31

2.2.5 Swali la 7: Matumizi ya Lugha ......................................................................................35

2.2.6 Swali la 8: Uhakiki wa Ushairi ......................................................................................39

2.2.7 Swali la 9: Fasihi Simulizi ......................................................................................43

2.3 SEHEMU C: MAJIBU MAREFU ......................................................................................47

2.3.1 Swali la 10: Simu ya Maandishi ......................................................................................47

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA ......................................................................................51

4.0 HITIMISHO ......................................................................................52

5.0 MAPENDEKEZO ......................................................................................53

KIAMBATISHO A ......................................................................................54

## DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili Mwaka 2024 kwa Somo la Kiswahili imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, wakuzamitaala, watungasera, na wadau mbalimbali wa elimu. Upimaji huu ulitathmini mihtasari ya Kidato cha Kwanza na cha Pili ili kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu hususani katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Majibu ya wanafunzi ni kiashiria halisi kinachotathmini iwapo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa wanafunzi maarifa stahiki katika elimu ya sekondari kwa kidato cha kwanza na kidato cha pili.

Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi **730,671** sawa na **asilimia 91.74** walifaulu. Ufaulu huu ulikuwa wa chini kwa **asilimia 3.42** ikilinganishwa na mwaka 2023, ambapo wanafunzi **660,969** sawa na **asilimia 95.19** walifaulu. Sababu zilizochangia wanafunzi wengi kufanya vizuri au kwa kiwango cha wastani ni pamoja na kuwa na umahiri wa kutosha katika mada nyingi zilizopimwa, kukidhi matakwa ya swali, na uelewa wa kutosha wa dhana mbalimbali za lugha na fasihi na kutumia lugha fasaha.

Aidha, wanafunzi wachache sawa na **asilimia 8.26** walipata alama hafifu. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kuwa na uelewa mdogo wa mada nyingi zilizopimwa na wengine kukosa maarifa ya kutosha ya dhana mbalimbali zilizopimwa. Vilevile, wanafunzi hao walishindwa kujibu kulingana na matakwa ya swali pamoja na uwezo mdogo wa kujieleza kwa lugha fasaha.

Taarifa hii itawawezesha viongozi wa elimu, walimu, wanafunzi, na wadau mbalimbali wa elimu kupata mbinu bora zitakazotumika kuinua ufaulu katika somo la Kiswahili hivyo kuongeza ufaulu katika upimaji ujao unaoratibiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika mchakato wa uandishi wa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Somo la Kiswahili kwa Kidato cha Pili uliofanyika mwezi Novemba mwaka 2024 ulikuwa na maswali kumi (10). Maswali hayo yaligawanyika katika sehemu A, B na C. Sehemu A ilihusu maswali ya kuchagua na kuoanisha; Sehemu B ilihusu maswali ya majibu mafupi; na sehemu C ilihusu swali la uandishi wa simu. Mada zilizotahiniwa katika sehemu zote zilikuwa *Sarufi, Ufahamu, Mawasiliano, Utumizi wa Lugha, Fasihi,* na *Uandishi*. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu zote. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu umezingatia kikamilifu muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Kidato cha Kwanza na kidato cha Pili.

Jumla ya wanafunzi 869,725 walisajiliwa kufanya upimaji lakini ni wanafunzi 769,158 sawa na asilimia 88.44 ndio walifanya upimaji huo. Kati yao, wavulana walikuwa 359,443 sawa na asilimia 46.73 na wasichana 437,715 sawa na asilimia 56.91. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi katika upimaji huu ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 730,671 sawa na asilimia 91.74 walifaulu kwa kupata daraja kuanzia A hadi D. Hata hivyo, ufaulu huu kwa mwaka 2024 umeshuka ikilinganishwa na mwaka 2023, ambapo asilimia 95.19 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata daraja kuanzia A hadi D. Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi kwa kila daraja kwa mwaka 2024 na 2023 umeoneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Wanafunzi kwa Mwaka 2024 na 2023**

| **Mwaka** | **Waliofanya** | **Ufaulu wa Madaraja kwa Asilimia** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **A** | **B** | **C** | **D** | **F** |
| 2023 | 695,269 | 4.24 | 9.95 | 49.96 | 31.04 | 4.81 |
| 2024 | 797,158 | 5.35 | 10.00 | 47.17 | 29.22 | 8.26 |

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa kulikuwa na mwachano mdogo wa ufaulu wa wanafunzi katika madaraja kwa mwaka 2023 na mwaka 2024. Ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka 2024 uliongezeka katika madaraja A na B kwa asilimia 1.11 na 0.05 mtawalia. Hata hivyo, ufaulu ulipungua katika madaraja C na D kwa asilimia 2.79 na 1.82 mtawalia. Aidha, kumekuwa

na ongezeko la asilimia 3.45 ya wanafunzi waliopata daraja F. Hali hii inaashiria kuwa ufaulu wa somo hili ulishuka kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023.

Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya ufaulu, ambavyo ni kiwango *kizuri*, *kiwango cha wastani* na *kiwango hafifu*. Kiwango kizuri cha ufaulu kimeanzia alama 65 hadi 100; kiwango cha wastani kimeanzia alama 30 hadi 64; na kiwango hafifu kimeanzia alama 0 hadi 29. Chati mbalimbali zimetumika kufafanua viwango hivyo. Aidha, rangi mbalimbali zimetumika kuwakilisha viwango vya ufaulu, ambapo rangi ya kijani imewakilisha kiwango kizuri; rangi ya njano imewakilisha kiwango cha wastani; na rangi nyekundu imewakilisha kiwango hafifu. Vilevile, sampuli za majibu sahihi na yasiyo sahihi ya wanafunzi zimeambatishwa.

Kwa ujumla, uchambuzi huu unalenga kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi, na wadau wengine wa elimu katika mkakati wa kuendelea kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili miaka ijayo.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya uchambuzi wa kina kwa kila swali na majibu yaliyotolewa na wanafunzi kwa kuonesha maswali yaliyojibiwa vizuri na yale yaliyojibiwa vibaya. Aidha, sababu za ufaulu kwa viwango mbalimbali zimeelezwa bayana kwa kila swali. Vilevile, sampuli za majibu ya wanafunzi kwa kila swali zimeambatishwa ili kuthibitisha maelezo yaliyotolewa.

### 2.1 SEHEMU A : MASWALI YA KUCHAGUA


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2), ambapo swali la 1 lilikuwa la kuchagua likiwa na vipengele kumi (10). Swali la 2 lilikuwa la kuoanisha maana za dhana za kisarufi zilizo katika Orodha A na dhana husika katika Orodha B. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 15.

#### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua

Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuelewa dhana mbalimbali zinazohusu mada za *Fasihi kwa Ujumla, Uhakiki wa Kazi za Kifasihi, Uundaji wa Maneno, Ufahamu,*

*Aina za Maneno, Uandishi wa Insha, Mawasiliano* na *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali*. Swali lilimtaka mwanafunzi kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo manne (A – D) kwa kila kipengele. Kila kipengele kilikuwa na alama moja, hivyo kufanya swali hili kuwa na jumla ya alama 10.

Wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 walifanya swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu, ambapo asilimia 91.25 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri na wastani kwa kupata alama kuanzia alama 3 hadi 10. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 1:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa asilimia 19.39 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri; asilimia 71.87 walifaulu kwa kiwango cha wastani; na asilimia 8.75 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Uchambuzi wa kina wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya wanafunzi (71.87%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Ufaulu huu unatokana na wanafunzi hao kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele kuanzia 3 hadi 6 kati ya 10 vya swali hili.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi wachache, sawa na asilimia 19.39 walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu kuanzia alama 7 hadi 10. Wanafunzi hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa mada mbalimbali zilizopimwa hivyo kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele kuanzia 7 hadi 10 vya swali hili. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi aliyechagua herufi za jibu sahihi katika vipengele vyote na kupata alama 10.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Mtunzi wa mashairi hutumia miundo ya aina mbalimbali ili kuipa upekee kazi yake. Upi ni muundo wa 'tarbia' kati ya ifuatayo?

A Mistari miwili kwa kila ubeti B Mistari mitatu kwa kila ubeti
C Mistari minne kwa kila ubeti D Mistari mitano kwa kila ubeti

[C]

(ii) Kati ya vipengele vifuatavyo ni kipi **hakihusiani** na maudhui ya kazi ya fasihi?

A Mafunzo B Mtazamo
C Msimamo D Msisitizo

[D]

(iii) Sentensi ipi kati ya zifuatazo imeundwa kwa kuunganisha sentensi mbili?

A Mwalimu ameingia darasani kufundisha.
B Mama alichota maji lakini yamemwagika.
C Shule yetu ya msingi ni kubwa na nzuri.
D Mvua na mawingu hutegemeana daima.

[B]

(iv) Kwa kawaida, habari iliyofupishwa huwa na idadi ipi ya maneno kati ya haya?

A Nusu ya maneno yote
B Theluthi ya maneno yote
C Robo ya maneno yote
D Robo tatu ya maneno yote

[B]

(v) Neno lipi linadhihirisha kauli ya kutendwa katika kitenzi?

A Pikia B Pikiwa C Pikika D Pikwa

[D]

(vi) Ni seti ipi inawakilisha kikamilifu muundo wa mfumo wa lugha yoyote?

A Sauti, silabi, maneno na sentensi
B Sauti, silabi, irabu na maneno
C Silabi, irabu, maneno na sentensi
D Sauti, irabu, konsonanti na maneno

[A]

(vii) Katika maneno yafuatayo, ni orodha ipi yenye aina moja ya maneno?

A Bata, nyumba, uvivu, Kigoma
B Bata, nyumba, kula, Kigoma
C Nyumba, nywele, uvivu, pika
D Nywele, pika, andika, bata

[A]

(viii) Tamathali ya semi inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia viunganishi huitwaje?
A Takriri B Sitiari C Tashihisi D Tashbiha

D

(ix) Jambo lipi kati ya yafuatayo ni muhimu kuzingatiwa katika uandishi wa insha?
A Kujua jina halisi la mwandishi wa insha
B Kujua barabara jambo linaloandikiwa insha
C Kujua wahusika wanaoandikiwa insha
D Kujua barabara mahali pa kuandikia insha

B

(x) Ipi ni sifa mahususi ya lugha ya mazungumzo?
A Matumizi ya ishara B Matumizi ya alama
C Matumizi ya ala D Matumizi ya lahaja

A

**Kielelezo Na. 1.1:** Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 1

Katika Kielelezo Na.1.1, mwanafunzi alichagua herufi za majibu sahihi katika vipengele vyote 10 na kuziandika katika visanduku alivyopewa kwa mujibu wa matakwa ya swali. Uchambuzi zaidi wa namna wanafunzi walivyojibu vipengele vya swali hili umefafanuliwa kama ifuatavyo:

(i) *Mtunzi wa mashairi hutumia miundo ya aina mbalimbali ili kuipa upekee kazi yake. Upi ni muundo wa "tarbia" kati ya ifuatayo?*
A *Mistari miwili kwa kila ubeti*
B *Mistari mitatu kwa kila ubeti*
C *Mistari minne kwa kila ubeti*
D *Mistari mitano kwa kila ubeti*

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Kifasihi* katika kipengele cha Uhakiki wa Ushairi na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kukumbuka miundo ya mashairi. Wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi *C Mistari minne kwa kila ubeti,* ambao ndio muundo wa tarbia unaotumika katika utunzi wa mashairi. Uchaguzi wa herufi ya jibu sahihi katika kipengele hiki ulitokana na wanafunzi hao kuwa na uelewa wa kutosha wa miundo ya mashairi.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi walichagua vipotoshi *A Mistari miwili kwa kila ubeti; B Mistari mitatu kwa kila ubeti;* na *D Mistari mitano kwa kila ubeti*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha ya miundo ya mashairi, hivyo kushindwa kutambua kuwa mistari minne ndio muundo sahihi wa mashairi ya tarbia. Kwa ujumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na kutotambua kuwa *A Mistari miwili kwa kila ubeti* ni muundo wa mashairi ya tathnia; *B Mistari mitatu kwa kila ubeti* ni muundo wa mashairi ya tathlitha; na *D Mistari mitano kwa kila ubeti* kuwa ni muundo wa mashairi ya takhimisa.

(ii) *Kati ya vipengele vifuatavyo ni kipi* **hakihusiani** *na maudhui ya kazi ya fasihi?*

A *Mafunzo*
B *Mtazamo*
C *Msimamo*
D *Msisitizo*

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Kifasihi* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kubainisha vipengele vya maudhui katika kazi za fasihi. Wanafunzi waliokuwa na umahiri wa kutosha wa vipengele vya uhakiki wa kazi za kifasihi walichagua herufi ya jibu sahihi *D Msisitizo* kuwa ni kipengele kisichohusiana na maudhui ya kazi ya fasihi.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi katika swali hili walichagua vipotoshi *A Mafunzo*; *B Mtazamo*; na *C Msimamo*, ambavyo ni vipengele mahususi vinavyohusu maudhui katika kazi za kifasihi. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na wanafunzi hao kukosa umahiri wa kutosha wa vipengele vya maudhui ya kazi ya fasihi. Wanafunzi hao hawakujua kuwa *mafunzo* ni kipengele cha maudhui kinachotumiwa na wasanii wa kazi za fasihi kufikisha ujumbe kwa hadhira; *mtazamo* ni namna au jinsi msanii anavyoitazama jamii yake; na *msimamo* ni maoni ya msanii juu ya jambo fulani. Kwa ujumla, wanafunzi hao walishindwa kutambua kuwa *msisitizo* ni istilahi ya lugha ya

Kiswahili yenye maana ya kuweka mkazo juu ya jambo fulani isiyohusiana kabisa na vipengele vya maudhui ya kazi za kifasihi.

(iii) *Sentensi ipi kati ya zifuatazo imeundwa kwa kuunganisha sentensi mbili?*

A *Mwalimu ameingia darasani kufundisha.*

B *Mama alichota maji lakini yamemwagika.*

C *Shule yetu ya msingi ni kubwa na nzuri.*

D *Mvua na mawingu hutegemeana daima.*

Swali lilitoka katika mada ya *Miundo ya Tungo* hususani mada ndogo ya *Aina za Sentensi*. Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa miundo ya sentensi za Kiswahili. Baadhi ya wanafunzi walijibu vizuri swali hili kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi *B Mama alichota maji lakini yamemwagika* kuwa ni sentensi iliyoundwa na sentensi mbili 'Mama *alichota maji'* na '*Maji yamemwagika*' zilizounganishwa na kiunganishi *lakini*.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua vipotoshi *A Mwalimu ameingia darasani kufundisha* ; *C Shule yetu ya msingi ni kubwa na nzuri;* na *D Mvua na mawingu hutegemeana daima*. Uteuzi wa vipotoshi hivi ulitokana na wanafunzi kutotambua kuwa sentensi katika vipotoshi vyote zimeundwa na kitenzi kikuu kimoja na au kitenzi kishirikishi na hazina viunganishi, hivyo kuwa sentensi moja. Kwa ujumla, uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na wanafunzi hao kushindwa kuelewa kuwa sentensi inayoundwa na sentensi mbili ina sifa ya kuwa na vitenzi vikuu viwili vinavyotoa taarifa mbili tofauti na zilizo kamili.

(iv) *Kwa kawaida habari iliyofupishwa huwa na idadi ipi ya maneno kati ya haya ?*

A *Nusu ya maneno yote*

B *Theluthi ya maneno yote*

C *Robo ya maneno yote*

D *Robo tatu ya maneno yote*

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Ufahamu wa Kusoma* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kufupisha habari kwa kuzingatia vigezo muhimu hususani idadi sahihi ya maneno. Wanafunzi waliojibu vizuri kipengele hiki walichagua herufi ya jibu sahihi *B Theluthi ya maneno yote*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha ya mambo muhimu ya kuzingatiwa katika kufupisha habari.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi katika kujibu kipengele hiki walichagua vipotoshi *A Nusu ya maneno yote*; *C Robo ya maneno yote*; na *D Robo tatu ya maneno yote*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na wanafunzi hao kukosa maarifa ya kutosha ya idadi sahihi inayozingatiwa katika kufupisha habari.

(v) *Neno lipi linadhihirisha kauli ya kutendwa katika kitenzi?*
A *Pikia*
B *Pikiwa*
C *Pikika*
D *Pikwa*

Swali lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua neno linalodhihirisha kauli ya kutendwa katika kitenzi. Wanafunzi waliofanya vizuri kipengele hiki walichagua herufi ya jibu sahihi *D Pikwa*; neno linalodhihirisha kauli ya kutendwa kutokana na kuundwa na kiambishi -*w*-. Uchaguzi wa kauli hiyo ulitokana na kuwa na maarifa ya kutosha ya kauli za vitenzi.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua vipotoshi *A Pikia*, *B Pikiwa,* na *C Pikika.* Uchaguzi huu ulitokana na kutoelewa kuwa katika kauli ya kutendwa, kitenzi huundwa na kiambishi -w-. Wanafunzi hawa walikosa umahiri katika mada ndogo ya *Mnyumbuliko wa Vitenzi vya Kiswahili* hivyo kutoelewa kuwa maneno *pikia*, *pikiwa*, na *pikika* yanadhihirisha kauli za *kutendea*, *kutendewa*, na *kutendeka* kwa kuwa na viambishi -*i*-, -*iw*-, na -*ik*- mtawalia.

(vi) *Ni seti ipi inawakilisha kikamilifu muundo wa mfumo wa lugha yoyote?*

A *Sauti, silabi, maneno, na sentensi*

B *Sauti, silabi, irabu, na maneno*

C *Silabi, irabu, maneno, sentensi*

D *Sauti, irabu, konsonanti, na maneno*

Swali lilitoka katika mada ya *Mawasiliano* na lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kuhusu muundo wa mfumo wa lugha. Baadhi ya wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *A Sauti, silabi, maneno, na* sentensi. Uchaguzi huu unaonesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha juu ya mada ya *Mawasiliano*. Hivyo, kutambua kuwa kipengele hicho ndio seti sahihi inayowakilisha kikamilifu muundo wa mfumo wa lugha yoyote.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa mfumo wa lugha. Wanafunzi hao walichagua vipotoshi *B Sauti, silabi, irabu, na maneno*; *C Silabi,* ir*abu, maneno, sentensi*; *D Sauti, irabu, konsonanti, na maneno*. Kwa ujumla vipotoshi hivyo vilikuwa na baadhi ya maneno yasiyohusiana na muundo wa mfumo wa lugha. Kwa mfano, neno *irabu* katika vipotoshi *B*, *C*, na *D* hudhihirisha sauti za lugha zinazotamkwa bila kuwepo kizuizi chochote kwenye mkondo wa hewa kutoka. Vilevile, neno *konsonanti* katika kipengele *D* ni aina ya sauti za lugha ambazo hutamkwa kwa kubana au kuzuia mkondo wa hewa.

(vii) *Katika maneno yafuatayo, ni orodha ipi yenye aina moja ya maneno?*

A *Bata, nyumba, uvivu, Kigoma*

B *Bata, nyumba, kula, Kigoma*

C *Nyumba, nywele, uvivu, pika*

D *Nywele, pika, andika, bata*

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Ubainishaji wa Aina Saba za Maneno* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kukumbuka aina za maneno katika lugha ya Kiswahili.

Wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *A Bata, nyumba, uvivu, Kigoma*. Uchaguzi huo ulitokana na wanafunzi hao kuonesha kuwa na uelewa wa kutosha wa aina za maneno, hivyo kutambua kuwa chaguo *A* ndio orodha sahihi yenye aina moja ya maneno ambayo ni nomino.

Hata hivyo, wanafunzi wengine walishindwa kujibu kwa usahihi kutokana na kukosa uelewa wa kutosha wa aina za maneno, hivyo kuchagua vipotoshi *B Bata, nyumba, kula, Kigoma*; *C Nyumba, nywele, uvivu, pika*; na *D Nywele, pika, andika, bata*. Uteuzi wa vipotosha hivyo ulitokana na wanafunzi hao kushindwa kubaini kuwa maneno *kula, pika,* na *andika* yaliyopo katika seti za vipotoshi hivyo si nomino bali ni vitenzi kinyume na matakwa ya swali hili.

(viii) *Tamathali ya semi inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia viunganishi huitwaje?*

A *Takriri*
B *Sitiari*
C *Tashihisi*
D *Tashibiha*

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi kubaini kwa usahihi vipengele anuai vya uhakiki wa kazi za fasihi. Wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *D Tashibiha,* ambayo ni tamathali ya semi inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia viunganishi.

Hata hivyo, wanafunzi wengine ambao hawakujibu kwa usahihi swali hili kwani walichagua vipotoshi *A Takriri, B Sitiari* na *C Tashihisi.* Uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na wanafunzi hao kukosa uelewa wa tamathali hizo, ambapo *takriri* ni mbinu ya kisanaa inayorudiarudia neno au kifungu cha maneno ili kuonesha msisitizo wa jambo; *sitiari* ni aina ya semi inayolinganisha vitu au hali mbili bila kutumia kiunganishi; na *tashihisi* ni semi inayokipa kitu kisicho na uhai uwezo wa

kutenda kama binadamu. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unadhihirisha kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu tamathali za semi, hivyo kushindwa kukidhi matakwa ya swali.

(ix) *Jambo lipi kati ya yafuatayo ni muhimu kuzingatiwa katika uandishi wa insha?*

A *Kujua jina halisi la mwandishi wa insha*
B *Kujua barabara jambo halisi linaloandikiwa insha*
C *Kujua wahusika wanaoandikiwa insha*
D *Kujua barabara mahali pa kuandikia insha*

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi wa Insha* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha. Wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *B Kujua barabara jambo halisi linaloandikiwa insha*. Wanafunzi hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa mada ya uandishi wa insha, hivyo kubainisha kwa usahihi jambo muhimu la kuzingatiwa katika uandishi wa insha.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki walichagua vipotoshi *A Kujua jina halisi la mwandishi wa insha*; C *Kujua wahusika wanaoandikiwa insha*; na *D Kujua barabara mahali pa kuandikia insha*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa jambo muhimu la kuzingatiwa katika uandishi wa insha ni kujua kikamilifu jambo halisi linaloandikiwa insha.

(x) *Ipi ni sifa mahususi ya lugha ya mazungumzo ?*

A *Matumizi ya ishara*
B *Matumizi ya alama*
C *Matumizi ya ala*
D *Matumizi ya lahaja*

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Lugha ya Kimazungumzo na Kimaandishi* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kuchambua sifa mahususi za lugha ya mazungumzo. Wanafunzi

waliojibu vizuri kipengele hiki walichagua herufi ya jibu sahihi *A Matumizi ya ishara* kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha juu wa sifa za lugha ya mazungumzo, hivyo kubaini kuwa matumizi ya *ishara* ni sifa mojawapo ya lugha ya mazungumzo.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua vipotoshi *B Matumizi ya alama*, *C Matumizi ya ala* na *D Matumizi ya lahaja*. Uteuzi wa kipotoshi *matumizi ya alama* ulitokana na wanafunzi hao kutojua kuwa hiyo si sifa mahususi ya lugha ya mazungumzo bali ni nyenzo muhimu katika uandishi wa insha. Kipotoshi *matumizi ya ala* hakikuwa sahihi kwa kuwa ni kipengele kinachoshughulikiwa katika tawi la sanaa la muziki ; na kipotoshi *matumizi ya lahaja* hakihusiani na lugha ya mazungumzo kwani chenyewe ni tofauti katika matamshi, maumbo, na matumizi ya maneno katika maeneo mbalimbali kwa lugha yenye asili moja. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyechagua herufi za majibu yasiyo sahihi katika vipengele vyote kumi na kupata alama 0.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Mtunzi wa mashairi hutumia miundo ya aina mbalimbali ili kuipa upekee kazi yake. Upi ni muundo wa 'tarbia' kati ya ifuatayo?
A Mistari miwili kwa kila ubeti B Mistari mitatu kwa kila ubeti
C Mistari minne kwa kila ubeti D Mistari mitano kwa kila ubeti
[B]

(ii) Kati ya vipengele vifuatavyo ni kipi **hakihusiani** na maudhui ya kazi ya fasihi?
A Mafunzo B Mtazamo
C Msimamo D Msisitizo
[B]

(iii) Sentensi ipi kati ya zifuatazo imeundwa kwa kuunganisha sentensi mbili?
A Mwalimu ameingia darasani kufundisha.
B Mama alichota maji lakini yamemwagika.
C Shule yetu ya msingi ni kubwa na nzuri.
D Mvua na mawingu hutegemeana daima.
[D]

(iv) Kwa kawaida, habari iliyofupishwa huwa na idadi ipi ya maneno kati ya haya?
A Nusu ya maneno yote
B Theluthi ya maneno yote
C Robo ya maneno yote
D Robo tatu ya maneno yote
[A]

(v) Neno lipi linadhihirisha kauli ya kutendwa katika kitenzi?
A Pikia B Pikiwa C Pikika D Pikwa
[A]

(vi) Ni seti ipi inawakilisha kikamilifu muundo wa mfumo wa lugha yoyote?
A Sauti, silabi, maneno na sentensi
B Sauti, silabi, irabu na maneno
C Silabi, irabu, maneno na sentensi
D Sauti, irabu, konsonanti na maneno
[C]

(vii) Katika maneno yafuatayo, ni orodha ipi yenye aina moja ya maneno?
A Bata, nyumba, uvivu, Kigoma
B Bata, nyumba, kula, Kigoma
C Nyumba, nywele, uvivu, pika
D Nywele, pika, andika, bata
[B]

(viii) Tamathali ya semi inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia viunganishi huitwaje?
A Takriri B Sitiari C Tashihisi D Tashbiha [B]

(ix) Jambo lipi kati ya yafuatayo ni muhimu kuzingatiwa katika uandishi wa insha?
A Kujua jina halisi la mwandishi wa insha
B Kujua barabara jambo linaloandikiwa insha
C Kujua wahusika wanaoandikiwa insha
D Kujua barabara mahali pa kuandikia insha
[A]

(x) Ipi ni sifa mahususi ya lugha ya mazungumzo?
A Matumizi ya ishara B Matumizi ya alama
C Matumizi ya ala D Matumizi ya lahaja
[D]

**Kielelezo Na. 1.2:** *Majibu* ya Mwanafunzi *yasiyo Sahihi katika Swali la 1*

Katika Kielelezo Na. 1.2, mwanafunzi alijibu vibaya swali na kupata alama 0 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha ya mada mbalimbali zilizopimwa katika swali hili.


### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji* na lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi wa kutambua maana ya dhana za kisarufi zinazotumika katika lugha ya Kiswahili. Swali lilikuwa na vipengele vitano na lilimtaka mwanafunzi kuoanisha maana za dhana za kisarufi zilizopo katika **Orodha A** na dhana husika katika **Orodha B** kama ifuatavyo:

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| *(i) Sehemu ya neno ambayo haibadiliki.* | *A Mofu* |
| *(ii) Umbo linalowakilisha mofimu.* | *B Mofu huru* |
| *(iii) Kipashio kidogo kabisa chenye maana katika neno.* | *C Mofimu* |
| *(iv) Maumbo ambayo hayawezi kujitegemea yakiwa pekee.* | *D Kiambishi* |
| *(v) Kipashio kinachoweza kuambatanishwa kwenye mzizi wa neno na kuunda neno jipya.* | *E Mofu tegemezi* |
| | *F Mzizi* |
| | *G Sarufi* |

Wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 waliofanya upimaji walijibu swali hili. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika

swali hili unaonesha kuwa wanafunzi 715,349 sawa na asilimia 89.74 walifaulu kwa kiwango kizuri hadi kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 5. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, asilimia 56.13 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 33.60 walifaulu kwa kiwango cha wastani, na asilimia 10.26 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa zaidi ya nusu ya wanafunzi yaani asilimia 56.13 walijibu vizuri swali hili na kupata alama kati ya 4 na 5. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kuonesha umahiri mkubwa katika mada ya *Uundaji wa Maneno* hivyo kuoanisha kwa usahihi maana za dhana za kisarufi katika Orodha A na dhana husika katika Orodha B. Aidha, walioanisha kwa usahihi vipengele vyote vitano, ambapo katika kipegele (i) *Sehemu ya neno ambayo haibadiliki* walibainisha kuwa ni *F Mzizi*; (ii) *Umbo linalowakilisha mofimu* kuwa ni *A Mofu*; (iii) *Kipashio kidogo kabisa chenye maana katika neno* kuwa ni *C Mofimu*; (iv) *Maumbo ambayo hayawezi kujitegemea yakiwa pekee* kuwa ni *E Mofu tegemezi*, na (v) *Kipashio kinachoweza kuambatanishwa kwenye mzizi wa neno na kuunda neno jipya* kuwa ni *D Kiambishi*. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi

aliyejibu vizuri swali hili kwa kukidhi matakwa ya swali na kupata alama zote 5.

| **Majibu** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
| **Orodha B** | F | A | C | E | D |

**Kielelezo Na. 2.1:** *Majibu Sahihi* ya Mwanafunzi *katika Swali la 2*

Katika Kielelezo Na. 2.1, mwanafunzi alioanisha kwa usahihi maana ya dhana za kisarufi zilizo katika *Orodha A* na dhana husika katika *Orodha B* hivyo kukidhi matakwa ya swali.

Aidha, wanafunzi 267,875 sawa na asilimia 33.60 walikuwa na ufaulu wa wastani kwani walipata alama kati ya 2 na 3. Wanafunzi hao walioanisha kwa usahihi maana za dhana mbili hadi tatu na dhana husika katika Orodha B. Hata hivyo, wanafunzi hao walishindwa kuoanisha kwa usahihi maana za dhana zingine kwa kuchagua herufi za majibu yasiyo sahihi ya maana za dhana katika Orodha A. Hali hii ilitokana na wanafunzi hao kuwa na uelewa hafifu wa maana za dhana za kisarufi walizopewa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu kwa usahihi vipengele (ii), (iv) na (v) kwa kuchagua herufi *A*, *E*, na *D* mtawalia lakini alishindwa kubainisha majibu sahihi katika vipengele (i) na (iii) kwa kuchagua vipotoshi *B Mofu huru* na *F Mzizi mtawalia*, ambazo si dhana zinazooana na maana zake katika vipengele hivyo ambazo (i) ni *F* (mzizi) na (iii) ni *C* (mofu). Mwanafunzi huyo hakutambua kuwa *mofu huru* ni umbo lisilogawanyika katika maumbo madogo zaidi bila kupoteza maana ya msingi. Pia, *mzizi* ni sehemu ya neno ambayo haibadiliki.

Hata hivyo, wanafunzi wachache sawa na asilimia 10.26 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili hivyo kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1. Hali hii ilitokana na wanafunzi hao kukosa maarifa ya kutosha ya maana za dhana za kisarufi hivyo kushindwa kuoanisha kwa usahihi maana ya dhana za kisarufi katika Orodha A na dhana husika kutoka Orodha B. Baadhi yao walishindwa kuoanisha kwa usahihi vipengele vyote vitano na

wengine walioanisha kwa usahihi kipengele kimoja pekee. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alishindwa kuoanisha kwa usahihi vipengele vinne kutokana na kuchanganya maana za kisarufi za dhana alizopewa ambapo katika kipengele (i) alichagua kipotoshi B *Mofu huru* badala ya F Mzizi. Uteuzi wa kipotoshi hicho ulitokana na kukosa uelewa wa dhana ya kisarufi katika kipengele hicho ambapo *mofu huru* ni maneno yanayoundwa na umbo moja lisiloweza kugawanyika katika maumbo madogo zaidi bila kupoteza maana ya msingi.

Kadhalika, mwanafunzi mwingine katika kipengele (v) alichagua kipotoshi *G Sarufi* ambayo ni mfumo wa kanuni za lugha mahususi zinazojibainisha katika fonolojia, mofolojia, sintakiksia, na semantiki. Hata hivyo, herufi ya jibu sahihi katika kipengele hicho ni *D Kiambishi* ambacho kazi yake kubwa ni kuambatishwa kwenye mzizi ili kuunda neno jipya. Kwa ujumla, majibu ya wanafunzi katika kundi hili yanaonesha kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha wa maana ya dhana za kisarufi zilizokuwa katika Orodha A na dhana husika zilizokuwa katika Orodha B. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili na kupata alama 0.

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | E | B | G | D | F |

**Kielelezo Na. 2.2:** *Majibu yasiyo Sahihi* ya Mwanafunzi *katika Swali la 2*

Katika Kielelezo Na. 2.2**,** mwanafunzi alishindwa kuoanisha kwa usahihi maana ya dhana ya kisarufi hata moja kati ya zilizokuwa katika Orodha A na dhana husika katika Orodha B.

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba (7) ya majibu mafupi. Kila swali lilikuwa na alama kumi (10) hivyo kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 70. Maswali yaliyopimwa katika sehemu hii yalitungwa

kutoka katika mada ya *Ufahamu*, *Uundaji wa Maneno, Mawasiliano, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali, Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi,* na *Fasihi kwa Ujumla*.

### 2.2.1 Swali la 3: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* hususani mada ndogo ya Ufahamu *wa Kusoma Kimya* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kuelewa kifungu cha habari. Swali lilimtaka mwanafunzi kusoma kifungu cha habari alichopewa kisha kujibu maswali yanayofuata. Kifuatacho ni kifungu cha habari alichopewa.

*Miti ina faida nyingi sana katika maisha ya binadamu. Nchi isiyo na miti ni sawa na mtu atembeaye bila kuvaa nguo. Ipo miti ya asili na mingine ni kupandwa, yote hiyo ina faida lukuki kwa maisha ya binadamu.*

*Ongezeko la watu duniani na kutokuwa na nishati mbadala kama vile gesi na umeme hasa sehemu za vijijini kumesababisha matumizi lufufu ya kuni na mkaa. Matumizi haya yametokana na ukosefu wa elimu ya utunzaji wa mazingira. Hali hii imesababisha jangwa kwa kuwa waswahili husema, "chovya chovya humaliza buyu la asali."*

*Miti ina faida kadhaa katika maisha ya kiumbe yeyote duniani. Miti hutupatia hewa safi tunayoivuta kila sekunde ya uhai wetu, kutengeneza fanicha, kutupatia matunda ili kutukinga na magonjwa na harufu ya miti ni dawa dhidi ya maadui mbalimbali kama vile nyoka.*


*Ukataji miti hovyo una madhara kama vile ukame, mmomonyoko wa udongo, uhaba wa hewa safi ya oksijeni na athari nyingine nyingi zinazoondoa uwepo wa viumbe hai na viumbe visivyo hai.*

*Kwa sasa serikali yetu imeanzisha kampeni mbalimbali za kulinda mazingira kama vile, "kata mti panda, "mti wa milenia"na "mtu mmoja miti mingi." Kampeni hizo hutolewa*

*katika redio, runinga na vyombo vingine vya habari. Ni jukumu la kila mtu kuitunza na kuilinda misitu yetu.*

Wanafunzi walipaswa kujibu vipengele vitano baada ya kusoma kifungu cha habari. Kipengele (a) (i) kilimtaka mwanafunzi kuandika kichwa cha habari kwa maneno matano; (ii) kilimtaka mwanafunzi kutoa sababu ya kuwapo kwa wimbi kubwa la ukataji wa miti; na (iii) kilimtaka mwanafunzi kubainisha matumizi manne ya miti. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kuelezea umuhimu wa kampeni mbalimbali zinazotolewa katika vyombo vya habari katika jamii; na kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi kufupisha habari aliyoisoma kwa maneno yasiyopungua 60 na yasiyozidi 70.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya upimaji. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 770,979 sawa na asilimia 96.72 walikuwa na ufaulu wa wastani na mzuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 10. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 3:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, asilimia 62.77 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri; asilimia 33.95 walifaulu kwa kiwango cha wastani, na asilimia 3.28 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Uchambuzi uliofanyika katika swali hili unaonesha kuwa, wanafunzi wengi (62.77%) walijibu vizuri swali hili kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vinne hadi vitano na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10 hivyo kuashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa mada ya *Ufahamu*. Kati yao, asilimia 0.8 walijibu kwa usahihi vipengele vyote vitano (a) hadi (c) na kupata alama zote 10. Katika kipengele (a) (i) waliandika kichwa cha habari sahihi kulingana na habari waliyosoma kama vile FAIDA ZA MITI; UTUNZAJI WA MITI; UTUNZAJI WA MAZINGIRA; na UMUHIMU WA MITI. Katika kipengele (a) (ii) walieleza kwa usahihi sababu ya kuwepo kwa wimbi kubwa la ukataji wa miti kuwa ni *ongezeko kubwa la watu*, *ukosefu wa elimu ya utunzaji wa mazingira* na *ukosefu wa nishati mbadala kama gesi na umeme*.

Aidha, katika kipengele (a) (iii) walibainisha matumizi sahihi manne ya miti kama vile *kutupatia hewa safi*, *hutumika kutengeneza fenicha*, *hutupatia matunda ili kujikinga na magonjwa*, na *harufu ya miti ni dawa dhidi ya maadui kama vile nyoka*. Katika kipengele (b) walieleza kwa usahihi umuhimu wa kampeni zinazotolewa katika vyombo vya habari kuwa ni *utunzaji wa mazingira*, *kutokata miti ovyo* na *kupanda miti ya kutosha*. Katika kipengele (c) walifupisha kwa usahihi habari waliyopewa kwa maneno yasiyopungua 60 na yasiyozidi 70 ; kwa kuzingatia mawazo makuu ya habari waliyopewa; kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha kiini cha habari; kuandika habari yenye mantiki; na kuzingatia alama za uandishi. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hii na kukidhi matakwa ya swali.

**Maswali**:

(a) Kutokana na habari uliyosoma;

(i) Andika kichwa cha habari kwa maneno yasiyozidi matano.

UMUHIMU WA KUPANDA MITI

(ii) Unafikiri kwa nini kumekuwa na wimbi kubwa la ukataji wa miti?

Kwasababu ya ongezeko la watu duniani na kutokuwa na nishati mbadala kama vile gesi na umeme hasa sehemu ya vijijini

(iii) Bainisha matumizi manne ya miti.

- Miti hutupatia hewa safi tunayoivuta kila sekunde ya uhai wetu.
- Miti hutumika kwaajili ya kutengenezea fanicha
- Mitii hutupatia matunda ili kutukinga na magonjwa
- Harufu ya miti ni dawa dhidi ya maadui mbalimbali kama vile nyoka.

(b) Kulingana na habari uliyosoma, kampeni mbalimbali zinazotolewa katika vyombo vya habari zina umuhimu gani katika jamii?

Kampeni hizo zina umuhimu mkubwa katika jamii kwasababu humsaidia mtu kulinda na kuitunza misitu yetu mfano pale mtu anapokata mti ni lazima apande mwingine ili kuendeleza misitu yetu "kata mti panda mti"

(c) Fupisha habari uliyosoma kwa maneno yasiyopungua 60 na yasiyozidi 70.

Miti ina faida nyingi sana katika maisha ya binadamu. Ongezeko la watu duniani na kutokuwa na nishati mbadala kumesababisha matumizi lufufu ya kuni na mkaa. Ukataji miti ovyo una madhara kwa viumbe hai na viumbe visivyo hai. Kwa sasa serikali yetu imeamisha kampeni za kulinda mazingra kama vile "kata mti panda mti", "mti wa milenea" na "mtu mmoja miti mingi". Kampeni hizo hutolewa katika vyombo vya habari.

**Kielelezo Na. 3.1:** *Majibu Sahihi* ya Mwanafunzi *katika Swali la 3*

Katika Kielelezo Na. 3.1, mwanafunzi alijibu vizuri vipengele vyote kwa kuandika kichwa cha habari kwa herufi kubwa na kisichozidi maneno matano; aliandika sababu sahihi za kuwapo kwa wimbi kubwa la ukataji miti; aliandika matumizi sahihi manne ya miti kulingana na habari aliyopewa; na aliandika umuhimu wa kampeni mbalimbali zinazotolewa katika vyombo vya habari. Aidha, alifupisha habari kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa ufupisho hivyo kupata alama za juu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 33.95 ya wanafunzi walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 kutokana na kujibu kwa usahihi vipengele viwili hadi vitatu. Baadhi yao walijibu kwa usahihi kipengele (a) (i) kwa kuandika kichwa cha habari waliyopewa kwa maneno yasiyozidi matano *UMUHIMU WA MITI* na kipengele (iii) walibainisha kwa usahihi matumizi ya miti kuwa ni *Hutupatia hewa safi tunayoivuta kila sekunde ya uhai wetu* lakini wengine waliandika matumizi yasiyo sahihi kama vile *Miti ina faida nyingi katika maisha ya binadamu*, *Miti ina faida katika maisha ya viumbe duniani*, na *Ukataji miti huzalisha mbao za kujengea*, majibu yasiyotokana na maudhui ya kifungu cha habari.

Vilevile, katika kipengele (b) baadhi walishindwa kueleza umuhimu wa kampeni mbalimbali zinaotolewa katika vyombo vya habari, badala yake waliorodhesha kaulimbiu za kampeni mbalimbali kama vile *Kata mti panda mti* na *mti wa milenia* bila kuonesha umuhimu wa kampeni hizo. Katika kipengele (c) waliandika ufupisho usiokidhi baadhi ya vigezo vya uandishi wa ufupisho kama vile kuandika ufupisho bila kuzingatia alama za uandishi, kuandika sentensi ndefu zisizo na mkato wala nukta au kunakili sehemu kubwa ya maneno kutoka kwenye habari waliyopewa badala ya kutumia maneno yao mwenyewe, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi wachache (3.28%) walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha ya mada ya *Ufahamu*. Wanafunzi hao

walishindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingi vya swali hili. Kwa mfano, baadhi yao walijibu kwa usahihi kipengele kimoja au viwili pekee na wengine walishindwa kujibu vipengele vyote vitano. Wanafunzi hao walikosa uelewa wa kifungu cha habari, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi hususani kwa kunakili baadhi ya maneno katika habari na kuyafanya kuwa kichwa cha habari. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika *MAISHA YA VIUMBE* na mwingine alinakili sentensi ya kwanza katika aya ya kwanza ya kifungu cha habari *Miti ina faida nyingi sana katika maisha ya binadamu*.

Aidha, katika kipengele (ii) mwanafunzi huyo alishindwa kuandika sababu ya kuwapo kwa wimbi kubwa la ukataji miti kwa kuelezea madhara ya ukataji miti kama vile *ukame, mmomonyoko wa udongo,* na *uhaba wa hewa safi ya aksijeni*. Pia, katika kipengele (iii) alibainsha matumizi manne ya miti yasiyo sahihi kama *kulinda misitu yetu***,** *hupandwa katika eneo* dogo, *elimu ya utunzaji wa mazingira* na *kata mti panda mti wa milenia* badala ya kuelezea matumizi sahihi ya miti kama vile *kutupatia hewa safi*, *kutengeneza fenicha*, na *kutupatia matunda na dawa dhidi ya maadui kama vile nyoka*.

Kipengele (b) mwanafunzi huyo alishindwa kuandika kwa usahihi umuhimu wa kampeni mbalimbali zinazotolewa katika vyombo vya habari badala yake aliandika *ni jukumu la kila mtu kuitunza na kuilinda misitu yetu*. Vilevile, katika kipengele (c) alinakili aya ya kwanza hadi ya tatu za habari aliyopewa badala ya kuandika ufupisho kwa maneno yake mwenyewe. Pia, mwanafunzi huyo hakuzingatia ipasavyo taratibu za uandishi wa ufupisho, hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vibaya swali hili kwa kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali.

**Maswali**:

(a) Kutokana na habari uliyosoma;

(i) Andika kichwa cha habari kwa maneno yasiyozidi matano.

miti inafaida nyingi katika maisha ya binadamu

(ii) Unafikiri kwa nini kumekuwa na wimbi kubwa la ukataji wa miti?

Kwasababu wanatumia Kuni na mkaa Katika sehemu ya vijijini

(iii) Bainisha matumizi manne ya miti.

- Kutengenezeamimbao
- Kutengenezea madawati
- Kutengenezea mabirisha
- Kutengenezea meza

(b) Kulingana na habari uliyosoma, kampeni mbalimbali zinazotolewa katika vyombo vya habari zina umuhimu gani katika jamii?

Kuelimisha Jamii au Kuelimisha msikili zaji wa habari

**Kielelezo Na. 3.2:** *Majibu yasiyo Sahihi* ya Mwanafunzi *katika Swali la 3*


Katika Kielelezo Na. 3.2**,** mwanafunzi alishindwa kuandika kichwa cha habari kwa herufi kubwa na kuzingatia idadi sahihi ya maneno ; alitoa sababu isiyojitosheleza ya kuwapo kwa wimbi kubwa la ukataji miti ; alibainisha matumizi ya miti yasiyoelelezwa kwenye habari aliyopewa ; na hakuelezea umuhimu wa kampeni mbalimbali zinazotolewa na vyombo vya habari kulingana na kifungu cha habari, hivyo kupata alama hafifu

### 2.2.2 Swali la 4: Uundaji wa Maneno

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kutambua dhima mbalimbali za viambishi katika vitenzi vya Kiswahili. Swali lilikuwa na vipengele vitano (a) hadi (e) na kila kipengele kilikuwa na vipengele vidogo viwili (i) na (ii). Swali lilimtaka

mwanafunzi kubainisha dhima mbili kwa kila kiambishi kilichokolezwa wino.

Wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango hafifu kwani wanafunzi wachache (185,220) sawa na asilimia 23.24 ndio waliofaulu kwa kiwango cha wastani na kizuri. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kiasilimia.





**Chati Na. 4:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, asilimia 0.89 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri; asilimia 22.35 walifaulu kwa kiwango cha wastani; na asilimia 76.76 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, wanafunzi 611,938 sawa na asilimia 76.76 walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Kiwango hiki cha ufaulu kilitokana na wanafunzi hao kukosa maarifa ya kutosha ya dhima za viambishi hivyo kushindwa kubainisha kwa usahihi dhima mbili za viambishi vilivyokolezwa wino katika vitenzi walivyopewa. Miongoni mwao, wanafunzi 220, 877 sawa na asilimia 27.71 walishindwa kubainisha dhima ya kiambishi hata moja, hivyo kupata alama 0. Baadhi yao walionesha kutoelewa maana ya istilahi *dhima* kuwa ni *kazi* badala yake walitoa maana kwa viambishi walivyopewa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika

kipengele (a) alieleza maana ya kiambishi **ta** kuwa ni silabi inayounda neno *atakuja* badala ya kubainisha dhima za kiambishi hicho kama (i) kiambishi cha wakati ujao na (ii) hali ya kutarajia. Pia, mwanafunzi mwingine alibainisha dhima ya viambishi **ta**, **u**, **m**, **ku** na **si** kama *mzizi* katika maneno husika hivyo kutotambua kuwa *mzizi* ni sehemu ya neno isiyobadilika, hivyo kupata alama 0.

Kadhalika, kwa kukosa umahiri wa kubainisha dhima sahihi katika viambishi, wanafunzi wengine walibainisha dhima zisizo sahihi katika vipengele vingi na wengine waliandika mambo yasiyohusiana na dhima za viambishi walivyopewa. Mathalani, mwanafunzi mmoja katika vipengele (a - e) alibainisha maana mbalimbali zilizokuwa katika vitenzi hivyo kama vile (a) *atakuja* - ujio wa mtu, (b) *umeanguka* - kupoteza mwelekeo, (c) *alimfundisha* - hali ya kumpa mtu elimu, (d*) ninakupenda* - hali ya kumwonesha mtu upendo, na (e) *sitaimba* - ukanushi wa kuimba, majibu yaliyo kinyume na matakwa ya swali. Wanafunzi hao walitakiwa kubainisha dhima anuai za viambishi walivyopewa kama ifuatavyo: (a) a***ta***kuja (i) kiambishi cha wakati ujao na (ii) hali ya kutarajia; (b) ***u***meanguka (i) kuonesha idadi (umoja) (ii) upatanisho wa kisarufi/kipatanishi cha ngeli U-ZI; (c) ali***m***fundisha (i) nafsi ya tatu/idadi (umoja) na (ii) mtendwa/yambwa; (d) nina***ku***penda (i) nafsi ya pili/idadi umoja (ii) mtendwa; na (e) ***si***taimba (i) ukanushi/nafsi ya kwanza umoja na (ii) mtenda. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama 0.


4. Katika kipengele (a) – (e), bainisha dhima mbili kwa kila kiambishi kilichokolezwa wino.

(a) Babu a**ta**kuja kesho asubuhi.

(i) Babu atakuja kesho asubuhi (maelezo)

(ii) Babu atakuja kesho asubuhi (swali?)

(b) Ukuta **u**meanguka.

(i) ukuta umeanguka (swali?)

(ii) ukuta umeanguka (mshangao!)

(c) Mwalimu ali**m**fundisha Bahati.

(i) Mwalimu alimfundisha Bahati (maelezo)

(ii) Mwalimu alimfundisha Bahati (swali?)

(d) Nina**ku**penda.

(i) Ninakupenda (maelezo)

(ii) Ninakupenda (mshangao!)

(e) **Si**taimba wimbo kesho.

(i) Sitaimba wimbo kesho (maelezo)

(ii) Sitaimba wimbo kesho (mshangao!)

**Kielelezo Na. 4.1:** *Majibu yasiyo Sahihi* ya Mwanafunzi *katika Swali la 4*


Katika Kielelezo Na. 4.1, mwanafunzi aliandika sentensi zenye kuonesha hali ya maelezo, swali, na mshangao katika maswali aliyopewa badala ya kubainisha dhima mbili za viambishi vilivyokolezwa wino katika vitenzi vilivyopo katika sentensi hizo.

Aidha, wanafunzi 178,111 sawa na asilimia 22.35 waliofanya swali hili walipata ufaulu wa wastani kuanzia alama 3 hadi 6. Ufaulu huu ulitokana na baadhi ya wanafunzi kubainisha dhima za viambishi katika vipengele viwili hadi vitatu walivyopewa. Wengine walibainisha dhima moja pekee katika kila kipengele badala ya mbili, hivyo kupata ufaulu wa wastani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache (0.89%) walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu kuanzia 6.5 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kuonesha umahiri wa hali ya juu katika mada ya *Uundaji wa Maneno* hususani mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji* hivyo kubainisha kwa usahihi

dhima mbili kwa kila kiambishi kilichokolezwa wino katika vipengele vyote vitano. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika katika kipengele (a) a**ta**kuja (i) kiambishi cha wakati ujao na (ii) hali ya kutarajia; (b) **u**meanguka (i) kuonesha idadi (umoja) na (ii) upatanisho wa kisarufi/kipatanishi cha ngeli U-ZI; (c) ali**m**fundisha (i) nafsi ya tatu/idadi (umoja) na (ii) mtendwa/yambwa; (d) nina**ku**penda (i) nafsi ya pili/idadi umoja na (ii) mtendwa; na (e) **si**taimba (i) ukanushi/nafsi ya kwanza umoja na (ii) mtenda.

Mwanafunzi mwingine alibainisha kwa usahihi dhima za viambishi hivyo kama ifuatavyo: (a) **ta** (i) *kudokeza njeo ya wakati ujao* na (ii) *kudokeza matarajio ya jambo fulani*; (b) **u** (i) *kudokeza ngeli ya **U-ZI*** na (ii) *kudokeza umoja*; (c) **m** (i) *kudokeza urejeshi wa mtendwa* na (ii) *kudokeza nafsi ya tatu umoja*; (d) **ku** (i) *kudokeza mtenda;* na (e) **si** (i) *kudokeza ukanushi* na (ii) *kudokeza nafsi ya kwanza umoja*. Hata hivyo, mwanafunzi huyo katika kipengele (d) (ii) aliandika dhima moja ya kiambishi **ku** kuwa ni *kusimama kama kiambishi cha katikati*, dhima ambayo si sahihi hivyo kupata alama 9. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili.


4. Katika kipengele (a) – (e), bainisha dhima mbili kwa kila kiambishi kilichokolezwa wino.

(a) Babu a**ta**kuja kesho asubuhi.
(i) -ta- Inadokeza njeo ya wakati ujao
(ii) Pia -ta- Inadokeza hali ya matarajio.

(b) Ukuta **u**meanguka.
(i) -U- Inadokeza ngeli
(ii) -U- Inadokeza Umoja maana yake Ukuta uliaanguka ni mmoja.

(c) Mwalimu ali**m**fundisha Bahati.
(i) -M- Inadokeza Mtendwa au Inarejelea mtendwa.
(ii) -M- Inadokeza nafsi ya tatu umoja.

(d) Nina**ku**penda.
(i) -ku- Inarejelea mtendwa
(ii) -ku- Inadokeza nafsi ya pili umoja.

(e) **Si**taimba wimbo kesho.
(i) -si- Inadokeza ukanushi.
(ii) si- Inadokeza nafsi ya kwanza umoja.


**Kielelezo Na. 4.2:** *Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 4*

Katika Kielelezo Na. 4.2, mwanafunzi alijibu kwa usahihi swali hili kwa kubainisha dhima mbili kwa kila kiambishi hivyo kukidhi matakwa ya swali na kupata alama za juu.

### 2.2.3 Swali la 5: Uundaji wa Maneno

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuunda maneno kwa kumtaka kubainisha shina la neno katika vitenzi alivyopewa katika vipengele (a) Analima, (b) Alipiga, (c) Wanacheza, (d) Kilianguka na (e) Atachapa.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya upimaji. Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha chini zaidi cha ufaulu kwa kuwa wanafunzi 156,439 sawa na asilimia 19.62 pekee ndio walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 5:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 5*


Chati Na. 5 inaonesha kuwa, asilimia 17.75 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 1.88 walifaulu kwa

kiwango cha wastani, na asilimia 80.38 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi (640,719) sawa na asilimia 80.38 walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Miongoni mwao, wanafunzi 627,105 sawa na asilimia 78.7 walipata alama 0 kwani walishindwa kabisa kubainisha shina hata moja katika vitenzi walivyopopewa. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kukosa umahiri wa uambishaji wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili. Baadhi yao, walibainisha kwa usahihi shina moja tu na kushindwa kubainisha kwa usahihi mashina manne ya maneno katika vitenzi walivyopewa. Wanafunzi wengine walibainisha mzizi katika vitenzi hivyo kama vile (a) -*lim*-, (b) -*pig*-, (c) -*chez*-, (d) -*anguk*-, na (e) -*chap*-.

Hali hii inaonesha kuwa wanafunzi hao walichanganya dhana ya *mzizi* wa neno na *shina* la neno kwa kuwa *mzizi* ni sehemu ya neno inayobaki baada ya kuondoa viambishi vyote katika neno husika na *shina* ni mzizi wa neno pamoja na kiambishi kiishirizi. Kukosa maarifa haya kuliwafanya washindwe kujua kuwa -*lim*-, -*pig*-, -*chez*-, -*anguk*- na -chap- ni mizizi ya maneno na si mashina kwa sababu haina viambishi viishirizi. Pia, wanafunzi wengine walibainisha kauli mbalimbali katika vitenzi walivyopewa kama vile *Limiana*, *Walipigana*, *Walichezesha*, *Kiliangukia* na *Watachapana*.

Vilevile, baadhi ya wanafunzi walibadilisha kategoria ya vitenzi walivyopewa na kuwa nomino kama vile (a) *kilimo*, (b) *pigo*, (c) *mchezo*, (d) *anguko*, na (e) *kichapo*. Wanafunzi wengine walishindwa kabisa kubainisha mashina ya maneno katika vitenzi kwenye vipengele vyote vitano vya swali hili. Kwa ujumla, wanafunzi walitakiwa kubainisha mashina katika vitenzi walivyopewa kama ifuatavyo: (a) *lima*, (b) *piga*, (c) *cheza*, (d) *anguka*, na (e) *chapa*. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 5.




5. Bainisha shina la neno katika vitenzi vifuatavyo:

(a) Analima ……-lim-……………………………………………………..
(b) Alipiga ……-pig-……………………………………………………
(c) Wanacheza……-chez-………………………………………………..
(d) Kilianguka……-anguk-……………………………………………
(e) Atachapa……-chap-………………………………………………..

**Kielelezo Na. 5.1:** *Majibu yasiyo Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 5*

Katika Kielelezo Na. 5.1, mwanafunzi alibainisha *mzizi* katika maneno aliyopewa badala ya *shina* kama swali lilivyotakiwa na kupata alama 0.

Uchambuzi wa kina wa majibu ya wanafunzi katika swali hili unaonesha kuwa wanafunzi 141,456 sawa na asilimia 17.74 walifanya vizuri swali hili na kupata alama za juu kuanzia 6.5 hadi 10. Ufaulu huo ulitokana na wanafunzi hao kuwa na umahiri wa kutosha wa mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji*. Wanafunzi hao walibainisha kwa usahihi shina la neno katika vitenzi walivyopewa kwenye vipengele vyote vitano. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alibainisha kwa usahihi mashina ya vitenzi katika vitenzi vyote vitano kuwa (a) *lima*, (b) *piga*, (c) *cheza*, (d) *anguka*, na (e) *chapa*. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote 10.



5. Bainisha shina la neno katika vitenzi vifuatavyo:

(a) Analima ……lima……………………………………………………..
(b) Alipiga ……piga……………………………………………………
(c) Wanacheza……cheza………………………………………………..
(d) Kilianguka……anguka……………………………………………
(e) Atachapa……chapa………………………………………………..

**Kielelezo Na. 5.2:** *Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 5*


Katika Kielelezo Na. 5.2, mwanafunzi alibainisha kwa usahihi mashina katika vitenzi alivyopewa katika vipengele (a) - (e) na kupata alama za juu.

Aidha, wanafunzi 14,983 sawa na asilimia 1.88 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Ufaulu huu wa wastani ulitokana na wanafunzi hao kubainisha kwa usahihi mashina ya maneno katika vitenzi viwili hadi vitatu kati ya vitano walivyopewa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alibainisha kwa usahihi baadhi ya mashina katika vitenzi (a) *Lima* na (b) *Piga* lakini alishindwa katika vipengele (c) (d), na (e) kwa kuandika *chez*, a*nguk*, na c*hap* mtawalia, kinyume na matwaka ya swali.

### 2.2.4 Swali la 6: Mawasiliano

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Lugha kama Chombo cha Mawasiliano* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuchambua sifa anuai za lugha ya Kiswahili. Swali lilimtaka mwanafunzi kufafanua sifa tano za lugha.

Uchambuzi wa kina wa majibu ya wanafunzi katika swali hili unaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi ulikuwa hafifu, ambapo wanafunzi 165,908 sawa na asilimia 20.81 ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri na kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 10**.** Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.





**Chati Na. 6***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, asilimia 4.2 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 16.29 walifaulu kwa kiwango cha wastani, na asilimia 79.19 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili unaonesha kuwa, wanafunzi 631,250 sawa na asilimia 79.19 walikuwa na ufaulu wa kiwango cha chini kwa kupata alama kuanzia 0 hadi alama 2.5. Miongoni mwao, wanafunzi 417,329 sawa na asilimia 52.4 walishindwa kufafanua sifa hata moja kati ya sifa tano za lugha, hivyo kupata alama 0. Wanafunzi hao walikosa uelewa wa kutosha wa mada ya *Mawasiliano* hususani mada ndogo ya *Lugha kama Chombo cha Mawasiliano*, hivyo kushindwa kufafanua kwa usahihi sifa tano za lugha. Baadhi yao, walielezea dhima za fasihi katika jamii kama vile *kuonya*, *kuburudisha*, na *kuelimisha*.

Wanafunzi wengine walifafanua dhima za lugha badala ya sifa za lugha kama swali lilivyomtaka. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa hoja zifuatazo: (a) *Lugha ni chombo kikuu cha mawasiliano*, (b) *Lugha huleta umoja*, (c) *Lugha huleta uhusiano katika jamii*, na (d) *Lugha huelimisha jamii*, na (e) *Lugha inaburudisha jamii* kinyume na matakwa ya swali. Wanafunzi hao walitakiwa kufafanua sifa za lugha, ambazo ni *lugha hutumiwa na binadamu kwa lengo la mawasiliano: maneno yanayotumiwa katika lugha hayana uhusiano wa moja kwa moja na virejelewa (unasibu); lugha huchanganuliwa kuanzia mofu, maneno, virai, vishazi na sentensi; lugha huzingatia utaratibu maalum matamshi, lugha hufuata misingi ya fonimu; lugha ina mpangilio unaoleta maana, kuanzia fonimu, neno, kirai, kishazi hadi sentensi;* na *lugha hujizalisha ili kupata maneno mapya yaani huchukua maneno kutoka lugha nyingine ili kuongeza msamiati.* Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama 0.



6. Fafanua sifa tano za lugha.

(a) Kuelewana katika mazungumzo yenu

(b) Meno kutokuwa na maana zaidi ya moja

(c) Kuto kuwa na matusi katika mazungumzo

(d) Lugha ina sifa ya kudokeza njeo

(e) Lugha ina sifa ya kudokeza wakati.

**Kielelezo Na. 6.1:** *Majibu yasiyo Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 6*

Katika Kielelezo Na. 6.1, badala ya kufafanua sifa tano za lugha, mwanafunzi alibainisha dhana mchanganyiko za matumizi ya lugha kinyume na matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache (36,047) sawa na asilimia 4.52 walijibu vizuri swali hili na kupata ufaulu wa juu kuanzia alama 6.5 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao walionesha kuwa na umahiri wa kutosha wa mada ya *Mawasiliano* hususani mada ndogo ya *Lugha kama Chombo cha Mawasiliano*. Wanafunzi hao walifafanua kwa usahihi sifa za lugha, na wengine walitoa mifano sahihi kulingana sifa anuai za lugha, hivyo kupata alama za juu. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alifafanua kwa usahihi sifa za lugha katika vipengele vinne kama kuwa (a) *Lugha huzaliwa, hukua, hufa*; (b) *Lugha huathiri na huathiriwa*; (c) *Lugha zote ni bora;* na (e) *Lugha hurithishwa*. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.

6. Fafanua sifa tano za lugha.

(a) Lugha hutumiwa na binadamu. Lugha hutumiwa na binadamu tu na haiwezi kutumiwa na viumbe wengine kama wanyama.

(b) Lugha ni sauti ya nasibu, lugha ni sauti ya nasibu kwasababu hakuna kikao kilichopangwa juu ya jinsi ya kutumia lugha.

(c) Lugha huzaliwa, hukuwa na hata kufa kwa sababu lugha ni kiungo hai hivyo ni lazima kuzaliwa, kukuwa na hata kufa (kupotea).


(d) Lugha hufungamana na maisha halisi ya watu, lugha hufungamana na maisha halisi ya watu fulani katika jamii husika.

(e) Lugha hujitosheleza kimaana, ili lugha iitwe lugha fulani lazima hiyo lugha husika ijitosheleze kimaana.

**Kielelezo 6.2:** *Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 6*

Katika Kielelezo Na. 6.2, mwanafunzi alijibu vizuri swali hili kwa kufafanua kwa usahihi sifa tano za lugha hivyo kukidhi matakwa ya swali na kupata alama za juu.

Hata hivyo, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 129,861 sawa na asilimia 16.29 walishindwa kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele au kutoa ufafanuzi usiojitosheleza wa sifa za lugha, hivyo kupata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao walifafanua kwa usahihi sifa mbili au tatu lakini walishindwa kutoa ufafanuzi unaojitosheleza kwa baadhi ya hoja. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alifafanua sifa ya lugha kuwa '*lugha huwa na uwili'* lakini hakutoa mfano wa uwili katika lugha yaani mtoaji na mpokeaji au mzungumzaji na msikilizaji. Kielelezo 6.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyebainisha sifa za lugha kwa usahihi lakini hakufafanua ipasavyo, hivyo kupata alama za wastani.


6. Fafanua sifa tano za lugha.

(a) Lugha Lazima Imuhusu binadamu

(b) Lazima iambatane na Vitamkwa viitwavyo fonimu.

(c) Lazima iwe na mpangilio unaoleta maana.

(d) Lazima ifuate taratibu za uandishi.

(e) Lazima iambatane na Sauti ya binadamu kutoka kinywani.

**Kielelezo 6.3:** *Majibu ya Wastani ya Mwanafunzi katika Swali la 6*

### 2.2.5 Swali la 7: Matumizi ya Lugha

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Rejesta* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kutumia lugha katika mazingira mbalimbali. Swali lilimtaka mwanafunzi kuelezea dhima tano za rejesta katika lugha.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji. Uchambuzi uliofanyika katika swali hili unaonesha kuwa ufaulu wa jumla ulikuwa wa wastani, kwa kuwa wanafunzi 457,707 sawa na asilimia 57.42 walifaulu kwa kiwango cha wastani na kizuri. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.

**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 7**

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.5 | 339,451 | 42.58 |
| 3.0 - 6.0 | 334,207 | 41.92 |
| 6.5 - 10 | 123,500 | 15.49 |


Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa, asilimia 15.49 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 41.92 walifaulu kwa

kiwango cha wastani, na asilimia 42.58 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Wanafunzi 334,207 sawa na asilimia 41.92 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Ufaulu wa wastani ulitokana na wanafunzi hao kutoa majibu yasiyojitosheleza kuelezea dhima tano za rejesta katika lugha. Baadhi yao walielezea kwa usahihi baadhi ya dhima za rejesta lakini walishindwa kuelezea dhima zingine, hivyo kupata alama za wastani. Pia, wapo wanafunzi walioeleza kwa usahihi dhima tatu pekee badala ya tano na kupata alama za wastani. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alieleza dhima sahihi kuwa (a) *Hurahisisha mawasiliano*, (b) *Kupamba mazungumzo*, na (c) *Kuficha ujumbe.* Hata hivyo, katika vipengele (d) na (e) aliandika *Kuendeleza utamaduni wa jamii husika* na *Kuelimisha jamii* mtawalia, ambazo si dhima za rejesta bali ni dhima za fasihi.

Wanafunzi wengine 339,451 sawa na asilimia 42.58 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5 kutokana na kukosa umahiri wa kutosha wa mada ndogo ya *Rejesta.* Wanafunzi hao walishindwa kuelezea kwa usahihi dhima tano za rejesta katika lugha. Miongoni mwao, wanafunzi 151,776 sawa na asilimia 19 walishindwa kabisa kuelezea dhima hata moja ya rejesta katika lugha, hivyo kupata alama 0. Wengine walielezea sifa za misimu kama vile *hutokana na utani katika jamii*, *kuzuka na kupotea,* na *hutunza historia ya jamii.*

Katika kundi hili, wapo wanafunzi walioelezea mambo yasiyohusiana na dhima za rejesta katika lugha. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa hoja kama vile (a) *Rejesta husaidia wafanya biashara kutangaza biashara zao;* (b) *Rejesta huwasaidia wafanyabiasha ndogo ndogo kupata wateja*; (c) *Rejesta husaidia lugha kueleweka katika makampuni na mashuleni*; (d) *Rejesta husaidia lugha wakati wa utamkaji*; na (e) *Rejesta husaidia watu kutangaza vitu*. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali na kupata alama 0.



7. Eleza dhima tano za rejesta katika lugha.

(a) Rejesta ya mgahawani

(b) Rejesta ya Shuleni

(c) Rejesta ya hospitalini


(d) Rejesta ya Kanisani

(e) Rejesta ya Sokoni

**Kielelezo Na. 7.1:** *Majibu yasiyo Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 7*

Katika Kielelezo Na. 7.1, mwanafunzi alitaja aina za rejesta badala ya kueleza dhima za rejesta katika lugha.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 123,500 sawa na asilimia 15.49 walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu kuanzia 6.5 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kuwa na umahiri wa kutosha wa mada ndogo ya *Rejesta*. Kati yao, wanafunzi 38,501 sawa na asilimia 4.8 walipata alama zote 10 kwa kuwa walieleza kwa usahihi dhima tano za rejesta katika lugha. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alielezea kwa usahihi dhima tano za rejesta katika lugha kuwa *hutumika kurahisisha mawasiliano kwa wahusika*; *hutumika katika kukuza lugha*; *hutumika kuficha jambo kwa wasiohusika*; *hutumika kupamba lugha;* na *hutumika kupunguza ukali wa maneno*. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.




7. Eleza dhima tano za rejesta katika lugha.

(a) Rejesta hutumika kupamba lugha, rejesta inatumika kupamba lugha pale ambapo wazungumzaji wanapotumia lugha ya mkato-kali inayowavutia wasikilizaji pamoja na watumiaji wake pia.

(b) Rejesta kutumika kama kitambulisho cha wazungumzaji; hii ni kwasababu kazi ambayo mtu anaifanya humwezesha kumtambua kwamba huyu ni nani mfano mtu anaposikia nani-wali kuku anajua tu kwamba ~~hy~~ huyu ni mamantilie.

(c) Rejesta inatumika kupunguza ukali wa maneno mfano pale madaktari na manesi wanapo sema mtoto wako-



tumejitahidi kadiri tuwezavyo lakini hatimaye amefariki hapo rejesta imepunguza ukali wa neno kuliko kusema amekufa.

(d) Rejesta kutumika kuficha jambo kwa watu wasiohusika mfano madaktari pamoja na manesi wanaposema mtoto wako tumempima lakini imegundulika anaugonjwa wa kisasa kwa mtu ambaye hahusiki hawezi kujua kwamba kaambiwa mtoto wake anaukimwi.

(e) Rejesta kutumika kurahisisha mawasiliano katika lugha ya kiswahili; rejesta kurahisisha mawasiliano pale wazungumzaji wanapotumia lugha ya mkato na inayoeleweka mfano wahudumu wa hoteli wanaposema nani wali kuku, mteja-mimi hapa hapo rejesta imeokoa muda na wameelewana.


**Kielelezo Na. 7.2:** *Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 7*

Katika Kielelezo Na. 7.2, mwanafunzi alijibu kwa usahihi kwa kutoa maelezo sahihi ya dhima za rejesta.

### 2.2.6 Swali la 8: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuchambua vipengele vya fani na maudhui katika shairi alilopewa. Swali lilimtaka mwanafunzi kusoma shairi alilopewa kisha kujibu maswali yanayofuata. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano na lilimtaka mwanafunzi katika kipengele (a) Kubainisha (i) muundo na (ii) mtindo ; (b) Kueleza dhamira ya mwandishi katika ubeti wa pili ; (c) Kueleza kwa ufupi ujumbe wa shairi; (d) Kutoa methali moja yenye maana sawa na methali *Mzaha mzaha, hutumbua usaha;* na (e) Kuandika kichwa cha shairi kisichozidi maneno matano na kisichopungua maneno matatu.

Uchambuzi wa kina wa takwimu za ufaulu wa swali hili unaonesha kuwa wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 waliofanya upimaji walijibu swali hili. Wanafunzi 589,508 sawa na asilimia 73.95 walikuwa na ufaulu wa kiwango cha wastani na kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 10. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 8*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, asilimia 22.84 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 51.11 walifaulu kwa


kiwango cha wastani, na asilimia 26.05 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa zaidi ya nusu ya wanafunzi walifanya swali hili (51.11%) walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Ufaulu wa wastani ulitokana na wanafunzi hao kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingine vya swali. Baaadhi yao walijibu kwa usahihi vipengele viwili au vitatu na kushindwa vingine au kutoa majibu yasiyojitosheza kulingana na kifungu cha ushairi walichopewa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika kipengele (a) alibainisha kwa usahihi (i) muundo wa shairi kuwa ni *tarbia* ambao huwa na mishororo minne kwa kila ubeti na (ii) alibainisha kwa usahihi mtindo wa shairi kuwa ni wa *kimapokeo* unaozingatia urari wa vina na mizani. Aidha, katika kipengele (d) aliandika methali moja yenye maana sawa na methali *Mzaha mzaha, hutumbua usaha* kuwa ni *Mchelea mwana kulia, hulia yeye*, na katika kipengele (e) aliandika kwa usahihi kichwa cha shairi kuwa ni MAISHA YA WATOTO WA MTAANI.

Hata hivyo, mwanafunzi huyo alishindwa kuelezea dhamira ya mwandishi katika kipengele (b) kwa kuandika *Kula au riziki ya watoto wa mtaani ipo jalalani wanakotafuta* badala ya kuandika dhamira sahihi ambayo ni *magumu wanayoyapata watoto wa mitaani*. Pia, katika kipengele (c) alishindwa kueleza ujumbe sahihi wa shairi hilo kwa kutoa maelezo kuhusu *miundo mbalimbali ya mashairi* badala ya kuelezea ujumbe ambao mwandishi aliutoa kupitia kifungu cha ushairi ambapo *aliasa taifa kukabiliana na ongezeko la watoto wa mitaani ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kama vile; wizi, uporaji*.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 182,072 sawa na asilimia 22.84 walifanya vizuri swali hili na kupata alama za juu kuanzia 6.5 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Wanafunzi hao walitoa majibu sahihi katika vipengele vingi vya swali. Kwa mfano,

mwanafunzi mmoja alijibu kwa usahihi vipengele vyote vitano, ambapo katika kipengele (a) alibainisha kwa usahihi (i) muundo wa shairi kuwa ni *tarbia wenye mishororo minne* na (ii) mtindo ni *wa kimapokeo* unaozingatia urari wa vina na mizani. Katika kipengele (b) alielezea kwa usahihi dhamira ya mwandishi katika ubeti wa pili kuwa ni *kuonesha magumu ya watoto wa mitaani ya kukosa chakula*, *hali inayowafanya wawe na tabia za kuomba omba*. Katika kipengele (c) alielezea kwa usahihi ujumbe wa shairi kuwa ni *ongezeko la watoto wa mitaani na changamoto wanazopitia*. Katika kipengele (d) aliandika methali sahihi yenye maaana sawa na methali "*Mzaha mzaha, hutumbua usaha*" kama ilivyotumika katika shairi alilopewa kuwa ni "*Mdharau mwiba, mguu huota tende*". Pia, katika kipengele (e) aliandika kichwa sahihi cha shairi alilopewa kisichozidi maneno matano na kisichopungua maneno matatu kuwa ni *WATOTO WA MITAANI*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali hili na kupata alama zote 10.


**Maswali**

(a) Bainisha;

(i) Muundo wa shairi:

shairi lina muundo wa tarbiya

(ii) Mtindo wa shairi:

Mtindo wa kimapokeo

(b) Eleza dhamira ya mwandishi katika ubeti wa pili.

dhamira ya mwandishi ni kuelezea maisha ya watoto wa mtaani wanaoyopatashida katika upataji chakula huko mtaani

(c) Eleza kwa kifupi ujumbe wa shairi hili.

shairi hili linafundisha kuwa watoto kuachiliwa ni kutafuta majanga na kusababisha ongezeko la watoto wa mitaani na waporaji, kwahiyo tunatakiwa kuwa makini na kuwasimamia watoto ipasavyo

(d) Toa methali nyingine moja yenye maana sawa na methali "Mzaha mzaha, hutumbua usaha" kama ilivyotumika katika shairi.

Usipoziba ufa utajenga ukuta

(e) Andika kichwa cha habari cha shairi hili kisichozidi maneno matano na kisichopungua maneno matatu.


WATOTO WA MITAANI

**Kielelezo Na. 8.1:** *Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 8*

Katika Kielelezo Na. 8.1, mwanafunzi alijibu kwa usahihi vipengele vyote vitano vya swali hili na kukidhi matakwa yote ya swali hivyo kupata alama za juu.

Hata hivyo, wanafunzi 207,650 sawa na asilimia 26.05 walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi, hivyo kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kukosa maarifa ya kutosha ya mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Baadhi yao walishindwa kujibu kipengele hata kimoja na wengine walijibu kipengele kimoja kati ya vipengele vitano na wengine walitoa majibu yasiyo sahihi ingawa walijibu vipengele vyote. Wapo wanafunzi waliobainisha dhamira mbalimbali katika shairi walilopewa kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja, katika vipengele (a), (b), (c) alinakili maneno yaliyopo kwenye shairi alilopewa badala ya kubainisha *muundo na mtindo*, *dhamira ya mtunzi*, na *ujumbe wa shairi* mtawalia. Katika kipengele (a) (i) aliandika *Watoto wa mtaani mada imeshafungua* na (ii) *Nawaonea huruma dunia imewatupa.* Katika kipengele (d) aliandika methali *Mtaka cha uvunguni, sharti ainame* isiyo na maana sawa na methali aliyopewa yaani *Mzahamzaha, hutumbua usaha*.

Mwanafunzi huyu hakutambua kuwa methali hiyo ina maana ya *Mtu yeyote anayetaka kufanikisha jambo sharti afanye bidii ili kukipata anachokitafuta* wakati methali "*Mzahamzaha, hutumbua usaha*" ina maana ya kuwa *jambo dogo unalolifanyia masihara linaweza kuleta madhara makubwa.* Pia, katika kipengele (e) aliandika *Watoto wa mtaani mada imeshafungua* ambacho si kichwa sahihi cha shairi alilopewa. Vilevile, aliandika kichwa cha shairi kwa herufi ndogo badala ya herufi kubwa kinyume na taratibu za uandishi wa kichwa cha shairi. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama 0.



**Maswali**

(a) Bainisha;

(i) Muundo wa shairi:

MZAHA MZAHA HUUTUMBUA USAHA

(ii) Mtindo wa shairi:

ABIRIA WANAJUA KILA KITU KIMEKOBURA

(b) Eleza dhamira ya mwandishi katika ubeti wa pili.

anaomba

Mazoea

huruma

Imani

Anakulilia

(c) Eleza kwa kifupi ujumbe wa shairi hili.

Mazoea Umkute Kituoni

(d) Toa methali nyingine moja yenye maana sawa na methali "Mzaha mzaha, hutumbua usaha" kama ilivyotumika katika shairi.

Mwenda pole hajikwai

(e) Andika kichwa cha habari cha shairi hili kisichozidi maneno matano na kisichopungua maneno matatu.

Mzaha Mzaha huutumbua Usaha

**Kielelezo Na. 8.2:** *Majibu yasiyo Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 8*


Katika Kielelezo 8.2, mwanafunzi alishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kwani alinakili maneno/vifungu vya maneno vilivyotumika katika shairi kinyume na matakwa ya swali.

### 2.2.7 Swali la 9: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Aina za Fasihi* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuchambua tofauti zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Swali lilimtaka mwanafunzi kubainisha tofauti tano zilizopo kati ya fasihi simulizi na andishi.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu katika swali hili unaonesha kuwa wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 walifanya upimaji. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo wanafunzi 632,256 sawa na asilimia 79.31 walifaulu kwa kiwango cha wastani na kizuri kwa kupata

alama kuanzia 3 hadi 10. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 8:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 9*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, asilimia 63.53 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 15.78 walifaulu kwa kiwango cha wastani, na asilimia 20.29 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Wanafunzi wengi sawa na asilimia 63.53 walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu kuanzia 6.5 hadi 10. Miongoni mwao, wanafunzi 335,582 sawa na asilimia 42.1 walionesha kwa usahihi tofauti zote tano na kupata alama zote 10 za swali hili. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa aina za fasihi, hivyo waliweza kubainisha kwa usahihi tofauti za msingi zinazodhihirika katika fasihi andishi dhidi ya fasihi simulizi kama vile *fasihi simulizi huandaliwa kwa muda mfupi* ambapo *fasihi andishi huchukua muda mrefu kubuniwa na kuandikwa; fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya masimulizi (mdomo)* lakini *fasihi andishi huwasilishwa kwa maandishi; fasihi simulizi hupokea mabadiliko ya papo kwa papo* lakini *fasihi andishi haipokei mabadiliko hadi toleo jingine; ushirikishwaji wa hadhira katika fasihi simulizi huwa ni wa ana kwa ana* lakini *hadhira kujitenga na mwandishi katika fasihi andishi; fasihi simulizi huhifadhiwa kichwani* lakini *fasihi andishi huhifadhiwa*

*katika maandishi*; fasihi simulizi huweza *kupoteza sanaa yake ya awali kwa kudondosha au kuongeza vipengele* lakini *fasihi andishi haiwezi kupoteza sanaa yake ya awali kutokana na kuwa kwenye maandishi;* na *fasihi simulizi haina gharama na humilikiwa na jamii nzima* lakini *fasihi andishi huwa na gharama ya karatasi na kalamu/uchapaji na ni mali ya mtunzi.* Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyebainisha kwa usahihi tofauti zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

9. Bainisha tofauti tano zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

(a) Fasihi simulizi hutolewa kwa njia ya mdomo na husikilizwa WAKATI fasihi andishi hutolewa kwa njia ya maandishi na husomwa.

(b) Fasihi simulizi inahusisha pande mbili ambazo ni fanani na hadhira WAKATI Fasihi andishi inahusisha pande mbili ambazo ni msomaji na msikilizaji.

(c) Fasihi simulizi ni hai kwamaana inahusisha matumizi ya vitendo na hisia WAKATI fasihi andishi si hai kwasababu inahusisha matumizi ya maandishi bila ya vitendo wala ishara na hisia.

(d) Fasihi simulizi hupokea mabadiliko ya papo kwa papo pale inapokuwa imekosewa WAKATI Fasihi andishi haipokei mabadiliko ya papo kwa papo Mabadiliko yake huchukua muda mrefu.

(e) Fasihi simulizi huweza kuwasilishwa muda wowote kulingana na fanani WAKATI Fasihi andishi haiwezi kuwasilishwa muda wowote inapokuwa imeandikwa huwekwa kwa ajili ya msomaji.

**Kielelezo Na. 9.1:** *Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 9*


Katika Kielelezo Na. 9.1, mwanafunzi alibainisha kwa usahihi tofauti tano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi na kupata alama za juu.

Aidha, wanafunzi 125,791 sawa na asilimia 15,78 ya waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Ufaulu huu wa wastani ulitokana na wanafunzi hao kubainisha kwa usahihi tofauti mbili au tatu kati ya tano na kushindwa kubainisha tofauti zingine. Miongoni mwao, wapo

walioelezea hoja sahihi lakini wakachanganya na hoja zinazoonesha mfanano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi, badala ya kuonesha tofauti zake kama swali lilivyotaka, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi 164,902 sawa na asilimia 26.69 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kukosa uelewa wa kutosha wa mada ya *Fasihi kwa Ujumla* hususani mada ndogo ya *Aina za Fasihi*. Baadhi yao walielezea dhima za fasihi kama vile *kuonya, kuburudisha na kuelimisha*, na wengine walielezea sifa za lugha kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alibainisha sifa za fasihi simulizi kama kuwa (a) *hufikisha ujumbe kwa njia ya matamshi ya mdomo,* (c) *nyenzo kuu ya mawasiliano,* na (e) *husambaa kwa muda mfupi*. Pia alibainisha sifa za fasihi andishi kama vile (b) *Hufikisha ujumbe kwa njia ya maandishi* na (d) *ni nyenzo kuu ya maandishi,* majibu ambayo si sahihi.

Vilevile, mwanafunzi mwingine alibainisha sifa sahihi za aina moja ya fasihi kama vile (a) *Fasihi simulizi ni kongwe*, (b) *Fasihi andishi ni changa*, (c) *Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo*, (d) *Fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi,* na (e) *Fasihi simulizi himilikiwa na watu wote wanaojua kusoma na wasiojua kuasoma.* Majibu haya hayaoneshi tofauti zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi kama swali lilivyowataka. Kwa ujumla, wanafunzi hao walitakiwa kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kuzingatia sifa zake katika utayarishaji, uwasilishaji, umiliki, gharama, upokeaji wa mabadiliko, uhifadhi, na hali ya fanani/hadhira kama swali lilivyotaka. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama 0.


9. Bainisha tofauti tano zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

(a) Zote huwa na fanani

(b) Zote hadhira na fanani wa naonana ana kwa ana.

(c) zote zina dumu kwa muda

(d) Zote zina zinawasilishwa mbile ya hadhira

(e) Zote ni mali ya jamii nzima...

**Kielelezo Na. 9.2:** *Majibu yasiyo Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 9*

Katika Kielelezo 9.2, mwanafunzi alishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuwa alionesha mfanano uliopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

## 2.3 SEHEMU C: MAJIBU MAREFU

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lililomtaka mwanafunzi kuandika simu ya maandishi. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 15.

### 2.3.1 Swali la 10: Simu ya Maandishi

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Simu* ya Maandishi na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa uandishi wa ujumbe unaotumwa kwa njia ya simu ya maandishi. Swali lilimtaka mwanafunzi kubadili barua ya kirafiki aliyopewa kuwa simu ya maandishi kwa kutumia maneno yasiyozidi 10.

Wanafunzi 797,158 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa asilimia 48.57 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha wastani na kizuri. Jedwali Na. 3 linaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.

**Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 10**

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 – 4.0 | 409,956 | 51.42 |
| 4.5 – 9.5 | 247,175 | 31.01 |
| 10 - 15 | 140,027 | 17.57 |

Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa, asilimia 17.57 ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 31.01 walifaulu kwa kiwango cha wastani, na asilimia 51.42 walifaulu kwa kiwango hafifu.

Uchambuzi wa kina unaonesha kuwa, wanafunzi 409,956 sawa na asilimia 51.42 walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kati ya 0 na 4 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha ya uandishi wa simu ya maandishi. Miongoni mwao, asilimia 35.8 walipata alama 0 kutokana na kushindwa kubadilisha barua ya kirafiki waliyopewa kuwa simu ya maandishi kwa kutumia maneno yasiyozidi 10. Wanafunzi wengine walikosa kabisa umahiri wa kuandika simu ya maandishi na badala yake waliandika barua ya kirafiki kinyume na matakwa ya swali.

Wengine walichora simu za viganjani na kunakili ndani yake ujumbe waliopewa katika barua. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alinakili maneno ya mwanzo katika barua ya kirafiki aliyotakiwa kuibadili kuwa simu ya maandishi kwa kuandika "*Mpendwa kaka haruna mashaka kwanza shikamoo! Habari za hapo nyumbani…*" badala ya kuandika simu ya maandishi kama swali lilivyotaka. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika barua ya kirafiki kinyume na matakwa ya swali.

Shule ya sekondari Mburu
S.L.P 2020
Nyasa
9/12/2014

Mpendwa dada Fatuma hamisi Kwanza shikamoo!
habari za hapa nyumbani natumaheni wote ni wazi.
mawa afya tere mimi huku shuleni sijambo na endelea vizuri
namasomo yangu ya hapa shuleni

Dhumuni ya kuandika barua hihi nikuku taarifa ya
kuwa kuta kuwa na mahafari apashuleni siku ya tarehe
16/12/2014 siku yaijumaa naomba uwaalike wale waapo
nyumbani na majirani waapo nyumbani na mwambie baba
na mama aposhuleni muda wasaa 3:00 Asubuhi
Naomba na uwasalimiene mala fiki zangu waaposhuleni
nawemyewe naomba uwaalike na malimuamesema tuchangie
pesa 80,000 na sale zetu Shati jeupe na skete ya bluu
naomba na pesa kwaajiri ya kununua viatu veupepe
Shilingi 30,000 na omba na pesa ya kura sikukuu
Tafadhali naomba muuzurie katika mahafari yangu
bila kukosa mtu ata mmoja kwenye mahafari hihi yaki
Jana wenu mpendwa wa kidato cha nne(4)

Kwaheri hayo tu
Mdogo wako
Salma hamisi

**Kielelezo Na. 10.1:** *Jibu Lisilo Sahihi la Mwanafunzi katika Swali la 10*

Katika Kielelezo Na. 10.1, mwanafunzi aliandika barua ya kirafiki badala ya kubadili barua aliyopewa ili kuwa simu ya maandishi.

Aidha, wanafunzi 247,145 sawa na asilimia 31.01 walipata alama za wastani kuanzia 4.5 hadi 9.5. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kuandika simu ambayo haikuzingatia taratibu zote za uandishi wa simu ya maandishi kama vile jina na anwani ya mwandikiwa simu, ujumbe na jina la mtuma ujumbe, kutumia herufi kubwa, na kuzingatia idadi ya maneno (10). Baadhi ya wanafunzi katika kundi hili waliandika simu kwa herufi kubwa, na walitumia maneno kumi kama swali lilivyotaka, lakini hawakuandika anuani ya mwandikiwa au jina la mwandishi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika simu ya maandishi kama ifuatayo:

HARUNA MASHAKA SHIKAMOO NINAOMBA HELA YA KARO IMEPOTEA SAFARINI SAMAHANI. Simu hii ya maandishi haikujitosheleza, hivyo alipata alama za wastani.

Hali kadhalika, wanafunzi 140,027 sawa na asilimia 17.57 walijibu vizuri swali hili na kupata ufaulu wa juu kuanzia alama 10 hadi 15. Wanafunzi katika kundi hili walikuwa na umahiri wa kutosha wa mada ya *Uandishi* hususani mada ndogo ya *Uandishi wa Simu*. Wanafunzi hao waliweza kubadili barua ya kirafiki waliyopewa na kuandika simu ya maandishi isiyozidi maneno kumi kwa kuzingatia *anuani ya mwandikiwa*, *taarifa/ujumbe iliokusudiwa*, *jina la mtuma ujumbe*, *kutumia herufi kubwa*, na *kuzingatia idadi ya maneno kumi*. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili na kukidhi matakwa ya swali.

HARUNA MASHAKA SLP 1010 KASULU NIMEIBIWA
KARO NITUMIE NEEMA MASHAKA

**Kielelezo Na. 10.2:** *Jibu Sahihi la Mwanafunzi katika Swali la 10.*

Katika Kielelezo Na. 10.2, mwanafunzi alibadili barua ya kirafiki kuwa simu ya maandishi kwa kuzingatia kanuni na taratibu zote stahiki za uandishi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika mada tano (5) zilizopimwa katika somo la Kiswahili unaonesha kuwa, mada za ufahamu na fasihi kwa ujumla zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Mada ya *Ufahamu* ilikuwa na kiwango kizuri zaidi cha ufaulu kwa asilimia 96.72 ikifuatiwa na mada ya *Fasihi kwa Ujumla* iliyokuwa na ufaulu wa asilimia 76.63. Aidha, mada tatu zilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, ambazo ni *Uandishi/Utungaji* (48.57%), *Sarufi* (44.20%), na *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* (39.712%).

Takwimu za ufaulu katika upimaji huu kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023 zinaonesha kuwa, mada ya *Ufahamu* (96.72%) imeendelea kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu, jambo linalodhihirisha kuwa wanafunzi wengi wamepata umahiri wa kutosha wa kusoma kwa ufahamu. Pia, mada ya *Fasihi kwa Ujumla* (76.63%) imekuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa ongezeko kubwa la asilimia 28.94 ikilinganishwa na mwaka 2023, ambapo ufaulu ulikuwa kwa asilimia 47.69. Hata hivyo, mada ya *Uandishi/Utungaji* (48.57%) imeshuka hadi kiwango cha wastani cha ufaulu kwa asilimia 43.39 kutoka kiwango kizuri cha asilimia 91.96 kwa mwaka 2023. Aidha, mada za *Sarufi* (44.20%) na *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* (39.12%) zimeendelea kuwa na kiwango cha chini cha ufaulu ikilinganishwa na mwaka 2023, ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 61.93 na 29.76 mtawalia.

Wastani wa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika mada zote kwa mwaka 2024 ni asilimia 61.05. Kiwango hiki kimeongezeka kwa asilimia 0.67 ikilinganishwa na mwaka 2023, ambapo wastani wa kiwango cha ufaulu kwa mada kilikuwa asilimia 60.38. Ongezeko dogo la ufaulu kwa mwaka 2024 linaashiria kuwa wanafunzi wengi walikuwa na upungufu wa umahiri katika baadhi ya mada zilizopimwa. Hali hii inasisitiza umuhimu wa kuimarisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi kwani viwango vya ufaulu katika mada nyingi bado havikuimarika ipasavyo kutoka mwaka 2023 hadi 2024.

Mada ya *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha* imeendelea kuwa na kiwango cha chini cha ufaulu kwa asilimia 29.76 na 39.12 kwa miaka 2023 na 2024 mtawalia. Licha ya mada hii kuwa na ufaulu wa chini kwa miaka miwili mfululizo, kumekuwa na ongezeko la ufaulu la asilimia

9.36 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023. Hali hii inaonesha kuwa kuna jitihada zinazoendelea kufanyika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa mada hiyo. Jitihada hizo zinapaswa kuendelea kutiliwa mkazo ili wanafunzi wengi wapate umahiri wa kutosha wa dhana nzima ya mawasiliano na matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Kukosekana kwa umahiri huo, kuliwafanya wanafunzi wengi kushindwa kufafanua sifa anuai za lugha na kutotambua umuhimu wa kutumia lugha kulingana na miktadha (rejesta). Aidha, mada za *Sarufi* na *Uandishi/Utungaji* zinatakiwa kutiliwa mkazo pia katika ufundishaji na ujifunzaji wake ili kuwajengea wanafunzi msingi mzuri wa kujieleza na kuwa mahiri katika matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Uchambuzi wa viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa mada mbalimbali kwa mwaka 2024 umebainishwa katika **Kiambatisho A**.

## 4.0 HITIMISHO

Upimaji wa Kidato cha Pili Mwaka 2024 katika somo la Kiswahili ulizingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili na maswali yote yalipimwa kwa kuzingatia nyanja za utambuzi ambazo ni *kuelewa, kukumbuka, kutumia, kuchambua, kutathmini* na *kuunda*. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi katika upimaji huu ulikuwa mzuri kwani asilimia 91.74 walifaulu.

Uchambuzi umeonesha mafanikio yaliyotokana na mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali kulikowafanya wanafunzi kujibu kwa usahihi maswali ya upimaji huu. Aidha, uchambuzi umeonesha changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika upimaji huu, kama vile baadhi ya wanafunzi kutokuwa na uelewa wa kutosha wa mada mbalimbali zilizopimwa hususani mada za *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha*, *Uandishi*, na *Sarufi*. Pia, kulikuwa na baadhi ya wanafunzi waliojibu maswali bila kuzingatia ipasavyo matakwa ya maswali. Ili kuimarisha viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili, changamoto hizi zinaweza kutatuliwa kwa kuwapa wanafunzi mazoezi ya kutosha na ya mara kwa mara ya sarufi, uandishi/utungaji, na mawasiliano na utumizi wa lugha katika mazingira mbalimbali.

Kwa kuzingatia ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika maswali yaliyopimwa katika mada mbalimbali kwa mwaka 2024, Baraza la Mitihani la Tanzania linatambua na kupongeza jitihada kubwa zinazoendelea kufanywa na wadau mbalimbali wa elimu nchini ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kidato cha Pili Mwaka 2024 inatarajiwa itumike ipasavyo ili kuwa chachu na dira ya mabadiliko kutoka viwango vya wastani vya ufaulu na kuwa viwango vizuri katika mada mbalimbali. Aidha, taarifa hii itawawezesha walimu, wanafunzi, na wadau wengine kuelewa changamoto mbalimbali zinazowakabili katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, hivyo kubuni mbinu na mikakati ya kuzitatua ili kuimarisha viwango vya ufaulu katika upimaji mwingine.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua zaidi ufaulu wa wanafunzi katika mada zilizokuwa na ufaulu wa wastani (*Uandishi, Sarufi,* na *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha*), walimu wanashauriwa :

(a) Kutumia vielelezo na zana za kufundishia zinazoakisi matumizi mbalimbali ya sarufi katika lugha ya Kiswahili hususani dhima za viambishi katika vitenzi vya Kiswahili.

(b) Kuongoza wanafunzi katika kufanya utafiti/kazi-mradi ili kuwajengea uelewa zaidi kuhusu dhana ya mzizi na shina la neno katika lugha ya Kiswahili.

(c) Kutumia mbinu ya igizo-dhima ili kuwawezesha wanafunzi kubaini mambo muhimu ya kuzingatiwa katika uandishi wa simu ya maandishi ili kuwajengea umahiri zaidi katika mada ya uandishi.

(d) Mada ya *Mawasiliano, Utumizi wa Lugha* na *Uandishi* zifundishwe kwa vitendo ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi kwa kulinganisha kinachofundishwa na matumizi halisi ya lugha katika jamii. Hili linaweza kufanyika kwa walimu kuanzisha mashindano ya darasa au shule ya uandishi pamoja na mijadala ili kuwazoesha wanafunzi kutumia kanuni za utumizi wa lugha na zana za mawasiliano.

**KIAMBATISHO A**

**UCHAMBUZI WA VIWANGO VYA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2024**

| Na. | Mada | Hali ya Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Na. ya Swali | % ya Ufaulu (Alama 30$^+$) | | |
| 1. | Ufahamu | 3 | 96.72 | 96.72 | Vizuri |
| 2. | Fasihi kwa Ujumla | 8 | 73.95 | 76.63 | Vizuri |
| | | 9 | 79.31 | | |
| 3. | Uandishi wa insha/ Simu | 10 | 48.57 | 48.57 | Wastani |
| 4. | Sarufi | 2 | 89.74 | 44.20 | Wastani |
| | | 4 | 23.24 | | |
| | | 5 | 19.62 | | |
| 5. | Mawasiliano na Matumizi ya Lugha | 6 | 20.81 | 39.12 | Wastani |
| | | 7 | 57.42 | | |